## Wawekezaji Pemba waguswa ziara ya Rais Dk. Mwinyi

**WAWEKEZAJI** mbalimbali ambao wamefungua milango ya kuwekeza katika kisiwa cha Pemba, wamefurahishwa na ziara ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi ...UK. 3



## PM aongeza wigo chanjo ya uviko 19

HABARI UK. 6


# UHURU

ISSN 0876 - 3896 Na. 23093 Jumatano Septemba 8, 2021 Tanzania sh 1,000

*Ukweli Daima*

@Uhuruonline Website: uhurumedia.co.tz


USIKOSE KUSOMA GAZETI LA UHURU VIJIJINI KESHOKUTWA

# Majaliwa ashusha nondo 7 Mifugo

- **AAGIZA** asilimia 15 mapato ya halmashauri yatokanayo na mifugo, yarejeshwe kuboresha miundombinu
- **AWATAKA** mawaziri Ummy wa TAMISEMI, Ndaki wa Mifugo na Uvuvi, wakutane kujadili namna bora ya utekelezaji
- **WIZARA** Uvuvi yatakiwa kusimamia mifumo ya masoko ili wafugaji wauze mifugo yao kwa bei yenye manufaa kwao

HABARI UK. 2

JOSHO



MAPATO



ARDHI





## Watakaovujisha mtihani darasa la saba kukiona

"Baraza la mitihani linawaasa walimu wakuu, waratibu elimu kata na wamiliki wa shule, kutojihusisha katika kupanga na kutekeleza njama za udanganyifu...

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Charles Msonde

ROYAL TOUR



**RAIS** Samia Suluhu Hassan.

## Machifu wafichua siri ya Rais Samia kusimikwa uchifu

UMOJA wa Machifu Tanzania (UMT), umetaja siri ya kilichowasukuma kumsimika Rais Samia Suluhu Hassan, kuwa Mkuu wa Machifu wote nchini, kwamba inatokana na imani kubwa waliyonayo juu ya kiongozi huyo mkuu wa nchi.

Pia, wametaja uamuzi wa Rais Samia kurekodi filamu ya kutangaza vivutio vya utalii nchini ukiwemo utamaduni wa Mtanzania, ambao unabeba matarajio... UK. 2

Scanned with CamScanner

# DAILY NEWS

## Standard 7 exams kick off today

SPORT



Govt to manage contracts for job seekers abroad

PAGE 2



Five new planes to boost pilot training

PAGE 4


INSIDE Academy

# PM debunks vaccine myths





## Broadband connectivity to reach all Tanzanians



8,319 km

## Govt pushes for value-added livestock products













Scanned with CamScanner

# majira

GAZETI HURU LA KILA SIKU

www.timesmajira.co.tz

ISSN 0856-5086 ■ NA. 9455 • VOL. II/8556
Jumatano 8 •SEPTEMBA • 2021
BEI: TSHS 1000/KSHS 60


## Mbaroni kwa tuhuma za kuuza watoto 11

Uk. 17

# Chadema yamtunishia msuli Jaji Mutungi

- **Ni pamoja na NCCR-Mageuzi, vyatoa tamko zito la kutohudhuria mkutano wake kumaliza mvutano na Polisi, vyasema havipo tayari kushiriki kuvunja Katiba** Uk. 4

## Askari Suma JKT matatani kwa tuhuma za mauaji

**Na Mwandishi Wetu, Arusha**

ASKARI watatu wa Suma JKT wanashikiliwa na Polisi mkoani Arusha kwa tuhuma za kumtesa hadi kumuua mkazi wa eneo la Ngaramtoni wilayani Arumeru...Inaendelea Uk. 4

## Wizara ya Mifugo yatwishwa zigo la migogoro ya ardhi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amefungua Mkutano wa Wadau wa Sekta ya Mifugo na ametumia fursa hiyo kutoa wito kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ishirikiane kikamilifu katika kutatua migogoro baina ya wafugaji na wakulima wengine wa ardhi...Inaendelea Uk. 4




## Uhaba vifaa tiba kuathiri ongezeko la wanachama CHF

UK. 16

# Wanafunzi mil. 1.1 kufanya mtihani darasa la saba leo

**Na Irene Clemence**

WATAHINIWA milioni 1,132,143 ambapo kati yao wavulana ni laki 547,502 sawa na asilimia 48.36, na wasichana 584,641 sawa na asilimia 51.64 wanatarajia kuanza kufanya mtihani wa kuhitimu darasa la saba kwa siku mbili kuanzia leo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani Tanzania (NACTE), Dkt. Charles Msonde, alisema watahiniwa hao...Inaendelea Uk. 4

## Mwanamke jela kwa kudhalilisha kingono mtoto wa kike

UK. 16

Scanned with CamScanner

nipashetz






**Mauaji** na unyama vyatikisa, askari Suma JKT mbaroni

UKURASA 2&3



Barca yamtaka Koeman kuwatumia Puig, Umtiti

UKURASA 21

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumatano Septemba 8, 2021



# Biashara watoto wauzwa 30,000/-

• **Wadaiwa** kupelekwa kwa wafugaji... *Endelea Uk. 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 5
**KANISA KATOLIKI LAONYA MADAKTARI**
RAIS wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Askofu Gervas...

UKURASA WA 5
**JELA MIAKA 10 KUMFANYIA UKATILI WA KINGONO MTOTO**
MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi wa Wilaya ya Igunga, mkoani...

UKURASA WA 7
**SERIKALI KUAMUA 'TUITION' SHULENI**
OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imea...



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akitazama viatu vilivyotengenezwa... Kilimanjaro International Leather Industries Company Limited... Julius Nyerere, Dar es Salaam, jana. **PICHA: PMO**

## Upelelezi tukio la Hamza kuvuka mipaka

UKURASA 3





# CHADEMA yamjibu msajili wa vyama, naye atoa neno

UKURASA 2

Scanned with CamScanner



HABARI KUTOKA BARA




# Majaliwa aitaka Wizara ya Mifugo kutatua migogoro

# Jela miaka 10 kwa kumbaka mtoto wa miaka minne

# Askari Suma JKT mbaroni kwa tuhuma za mauaji

Scanned with CamScanner

## MAZUNGUMZO



WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (Kulia), akizungumza na Mratibu wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFISH), Nichrous Mlalila (katikati) na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), Dk. Ishmael Kimirei, Makao Makuu ya TAFIRI, Dar es Salaam. (Picha na Wizara ya Mifugo na Uvuvi).

Scanned with CamScanner

300>> Idadi ya wadau ambao walihudhuria mkutano wa sekta ya mi

# Majaliwa ashusha nondo 7 Mifugo

**SWAUMU HASSAN (DSJ), SAMIRA OMARY (TUDARCo) Na JUMA ISSIHAKA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa maagizo saba kwa taasisi, mamlaka na Idara mbalimbali za serikali ili kuimarisha ustawi wa sekta ya mifugo na kuifanya itoe mchango chanya kwa taifa.

Maagizo hayo aliyatoa jijini Dar es Salaam jana, wakati akifungua mkutano wa wadau wa sekta ya mifugo uliofanyika katika Kituo cha Mikutano ya Kimataifa cha Julius Nyerere.

Maagizo au nondo hizo saba zilizotolewa maagizo na waziri mkuu ni hizi:

ASILIMIA 15 YA MAPATO

Majaliwa aliiagiza mamlaka ya serikali za mitaa, kuhakikisha asilimia 15 ya mapato ya halmashauri yatokanayo na mifugo, yanarudishwa ili kuboresha miundombinu ya sekta hiyo katika halmashauri husika.

"Mamlaka za serikali za mitaa, simamieni halmashauri zile asilimia 15, zitengwe na zirudi katika mifugo huko huko katika halmashauri, hii itasaidia kuwahamasisha wafugaji kuona kuwa, huduma zinatoka," alisema.

Katika utekelezaji wa hilo, aliwataka Waziri wa Mifugo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kukutana na kujadili namna nzuri ya kufanya.

**UKARIBU NA SEKTA BINAFSI**

Aliwaagiza viongozi na watendaji wa serikali, kuhakikisha wanakuwa karibu na sekta binafsi, kwa maana wafugaji ili kuwawezesha kuwekeza katika sekta ya mifugo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu yake.

"Hii ni kama vile kupata majosho, rambo, visima vya maji ili kufanya mifugo ishamiri ikiwa na afya njema," alisisitiza.

Aidha, aliiagiza TAMISEMI kushirikiana na sekta binafsi katika kutenga, kupima, kusimamia na kuendeleza maeneo ya malisho, kwa kufanya hilo, hakutakuwa na migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

KUBORESHA MIFUGO

Kwa mujibu wa Majaliwa, TAMISEMI inapaswa kuwahamasisha wafugaji kuboresha mifugo yao, ili kuongeza tija katika uzalishaji kupitia uhimilishaji, upandishaji wa madume na mitamba bora.

**TAASISI ZA UTAFITI**

Majaliwa aliziagiza Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kuhakikisha zinasimamia uboreshaji wa miundombinu ya taasisi zao za utafiti ambazo ni TARI na TARILI na kuzipatia fedha ili zifanye utafiti wenye tija kwa sekta ya mifugo.

Alitaka uhusiano wa kitaalamu kati ya taasisi hizo uimarishwe ili kutoa matokeo mazuri ya tafiti na kila utafiti urudi kwa walaji na wautumie kupata manufaa zaidi.

"Taasisi zinazozalisha na usambazaji wa mbegu bora za mifugo, ziendelee kuimarishwa ili kuongeza tija zaidi katika sekta hiyo na kuhamasisha wafugaji kutumia mifugo bora iliyofanyiwa utafiti kuonyesha kuwa na tija zaidi," alisema.

MASOKO

Aliitaka wizara husika kusimamia mifumo ya masoko, ili wafugaji wauze mifugo yao kwa bei nzuri ikiwemo kuimarisha ushirika wa wafugaji.

"Wafugaji hawa ili wafikiwe kwa ukaribu, waunde umoja wao wapambanue changamoto zao, wawasilishe kwa pamoja badala ya kila mmoja kuwa sehemu yake, haitakuwa rahisi kuwafikia, wakiwa na ushirika inakuwa rahisi zaidi," alisema.

Alisema hamasa hiyo ya kuundwa kwa ushirika katika mifugo inatokana na mafanikio yaliyoonekana katika kilimo.

**MIGOGORO**

Aliiagiza Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kuhakikisha inashiriki kikamilifu kutatua migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, wafanye hivyo kwa kuwaelimisha wafugaji kufuga kulingana na maeneo waliyonayo.

Pia, alizitaka halmashauri zisimamie na zihamasishe ufugaji ambao hautachochea migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

"Kumekuwa na malalamiko kwamba, wapo wafugaji wenye ng'ombe walioshikiliwa zaidi ya 5,000, wizara ni muhimu kupata taarifa hizi wapi mifugo imeshikiliwa na kama hakuna suluhu, lazima mwende kwa haraka sana kusikiliza kuna nini.

"Wakati mwingine watendaji wetu ni waonevu tu, wanataka kuwaonea wafugaji, jambo ambalo siyo sahihi, lakini pale ambapo hawafanyi vizuri bora waambiwe," alisema.

Hata hivyo, aliagiza kuachiwa kwa mifugo yote inayoendelea kushikiliwa ilhali Mahakama imeshaamuru iachiwe.

"Kama Mahakama imesema ng'ombe hawa hawana hatia, waachiwe ili mfugaji achukue ng'ombe wake akajipange vizuri, kama kuna kasoro ya kutojua mipaka tulishaagiza maeneo yote yatambue mipaka," aliongeza.

Alielekeza oparesheni za mifugo zifanywe kwa weledi, huku akiwasisitiza wafugaji kuacha kuingia katika maeneo waliyozuiliwa kuingia.

**SENSA YA MIFUGO**

Aliitaka mikoa yote nchini, kufanya sensa ya mara kwa mara, kutambua wafugaji wako wapi, wangapi na wana mifugo kiasi gani ili kuwezesha uratibu wa mifugo hiyo.

"Nilimuona Mkuu wa Mkoa wa Lindi, moja ya taarifa alisema walikuwa na wafugaji wengi walioingia huko, alichokifanya ni kuwatambua ni kina nani, wana mifugo kiasi gani na wapo maeneo gani kisha kuwapangia," alisema.

Alisisitiza elimu ya ufugaji bora kutolewa kwa wafugaji ili kuepuka ufugaji wa mifugo mingi isiyo na tija.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema mkutano huo umehudhuriwa na wadau zaidi ya 300, huku ukiwa na dhamira ya kupeana taarifa kuhusu fursa, changamoto na kujadili namna ya kukabiliana nazo.

Mkutano huo, umebeba kauli mbiu isemayo 'Kufikia Tanzania ya Viwanda 2025, ushiriki wa sektra binafsi katika sekta ya mifugo ni nguzo muhimu kuinua uchumi na kuongeza ajira'.

Scanned with CamScanner

## Wawekezaji Pemba waguswa ziara ya Rais Dk. Mwinyi

WAWEKEZAJI mbalimbali ambao wamefungua milango ya kuwekeza katika kisiwa cha Pemba, wamefurahishwa na ziara ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi ...UK. 3



## PM aongeza wigo chanjo ya uviko 19

HABARI UK. 6


# UHURU

USIKOSE KUSOMA GAZETI LA UHURU VIJIJINI KESHOKUTWA

ISSN 0876 - 3896 Na. 23093 Jumatano Septemba 8, 2021 Tanzania sh 1,000

Ukweli Daima

@Uhuruonline Website uhurumedia.co.tz




# Majaliwa ashusha nondo 7 Mifugo

- **AAGIZA** asilimia 15 mapato ya halmashauri yatokanayo na mifugo, yarejeshwe kuboresha miundombinu
- **AWATAKA** mawaziri Ummy wa TAMISEMI, Ndaki wa Mifugo na Uvuvi, wakutane kujadili namna bora ya utekelezaji
- **WIZARA** Uvuvi yatakiwa kusimamia mifumo ya masoko ili wafugaji wauze mifugo yao kwa bei yenye manufaa kwao

HABARI UK. 2

JOSHO



MAPATO



ARDHI



## Watakaovujisha mtihani darasa la saba kukiona

"Baraza la mitihani linawaasa walimu wakuu, waratibu elimu kata na wamiliki wa shule, kutojihusisha katika kupanga na kutekeleza njama za udanganyifu...

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Charles Msonde.

ROYAL TOUR



...S Samia Suluhu Hassan.

## Machifu wafichua siri ya Rais Samia kusimikwa uchifu

UMOJA wa Machifu Tanzania (UMT), umetaja siri ya kilichowasukuma kumsikimika Rais Samia Suluhu Hassan, kuwa Mkuu wa Machifu wote nchini, kwamba inatokana na imani kubwa waliyonayo juu ya kiongozi huyo mkuu wa nchi.

Pia, wametaja uamuzi wa Rais Samia kurekodi filamu ya kutangaza vivutio vya utalii nchini ukiwemo utamaduni wa Mtanzania, ambao unabeba matarajio... UK. 2

## ...skari watatu SUMA JKT mbaroni tuhuma za mauaji

UK. 3

Scanned with CamScanner




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akikagua mkanda uliotengenezwa kwa ngozi wakati wakipewa maelezo na Ofisa wa Masoko wa Kiwanda cha Kilimanjaro International Leather, Fredrick Njoka (kulia) alipotembelea banda lao kabla ya kufungua mkutano wa wadau wa sekta ya mifugo uliofanyika kwenye Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere jijini Dar es Salaam jana. **Picha na Sunday George**

# 'Wafugaji msiwape watoto kuchunga'

**Bakari Kiango**, Mwananchi
bkiango@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa amekemea vitendo vya baadhi ya wafugaji wanaowapa watoto ng'ombe kuwachunga, akisema si sahihi kwa sababu hawana uwezo wa kukaa na kundi kubwa la mifugo.

"Tuache tabia ya kuwapa watoto wadogo kuchunga ng'ombe, kwa sababu wanatakiwa kwenda shule, pili hawana uwezo wa kukaa na kundi kubwa. Najua utamaduni huko hivyo, lakini tuweke mwelekeo mzuri wa ufugaji," alisema Majaliwa.

Majaliwa alitoa kauli hiyo jana, wakati akifungua mkutano wa wadau wa sekta ya mifugo uliondaliwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mkutano uliwashirikisha baadhi wa wakuu wa mikoa ya Tanga, Pwani, Iringa, Lindi, Dar es Salaam, Manyara na Tabora.

Aliwataka wafugaji kuwakabidhi mifugo vijana wenye uwezo wa kutafakari na kujua namna ya kutekeleza vyema shughuli ya kuchunga na endapo ng'ombe akienda ndivyo sivyo, ni rahisi kumrudisha katika njia yake.

Katika mkutano huo, Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT), Jeremiah Wambura alimuomba Majaliwa kuingilia kati sakata la ng'ombe 5,000 wanaoshikiliwa katika hifadhi mbalimbali, zikiwamo za Meatu na Burigi, licha ya Mahakama kuamuru ziachiliwe.

"Tunaomba utusaidie mifugo hii iachiwe kwa sababu ng'ombe wanashikiliwa huku ndama wanaachwa wakifa. Waziri Mkuu, hatuwezi kupata maziwa kama ng'ombe wanashikiliwa," alisema Wambura.

Akijibu ombi hilo, Majaliwa alisema, "kama Mahakama imesema ng'ombe hawana hatia waachiwe ili mfugaji achukue mfugo wake na kujipanga vizuri katika maeneo yake.

Kama kuna mfugaji hapa ng'ombe wake wameshikiliwa baada ya tamko hili wamuone waziri," alisema Majaliwa.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alimuomba Majaliwa kuagiza wakuu wa mikoa kutekeleza waraka wa mwaka 2002 unaolekeza halmashauri kutenga asilimia 15 ya mapato yanatokanayo na mifugo, kisha zitumike kuboresha sekta hiyo.

**"Huko Lindi juzi wakulima wawili wameuawa na wafugaji, sio jambo jema, sababu ng'ombe amepelekwa katika shamba la mahindi. Ni vizuri kila mmoja aheshimu shughuli ya mwenzake [ili] tuishi vizuri katika jamii yetu."**
Kassim Majaliwa

SHERIA

# Mawakili 3,190 ...

Scanned with CamScanner

NDANI >> NDUGU WANNE MBARONI TUHUMA KUUA, KUKATA VIUNGO

ISSN 1821-570X
TOLEO NA. 09183
JUMATANO SEPTEMBA 8, 2021
TSH. 1,000
KSH. 100
www.habarileo.co.tz

# HabariLEO

GWIJI LA HABARI TANZANIA

## VIJANA 600 WAITWA USAILI POLISI DODOMA

UK 3

## WATENDAJI WAPEWA MAAGIZO 10 KUBORESHA MIFUGO

UK.3

# Majaliwa: Mkachanje acheni maneno

HABARI KAMILI UK.2



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na wadau wa sekta ya mifugo [illegible] uliofanyika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere, Dar es Salaam jana. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu).

## VIJANA WAWILI MBARONI WIZI WATOTO 11

- Waliwauza 25,000/- hadi 30,000/- kwa wafugaji

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linawashikilia watu watano kwa tuhuma mbalimbali wakiwemo wawili wanaotuhumiwa kujihusisha na biashara ya usafirishaji wa binadamu na kuwatumikisha watoto.

»UK.3


# Watahiniwa la saba waongezeka 10.6%

- Waanza mitihani leo, wawili mbaroni kuiba

HABARI UK.2

## KESI YA MBOWE YAPATA JAJI MWINGINE

»UK.3



859.3 >>> Kilo za dawa za kulevya mchanganyiko zilizokamatw

# Waziri Ndaki aipa maagizo TAFIRI ifanye kazi kwa tija

Na MWANDISHI WETU

TAASISI ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), imetakiwa kufanya kazi zenye tija kwa jamii na kutoa ushauri wa kisayansi namna ya kuhakikisha sekta ya uvuvi inakua na kusaidia Watanzania katika masuala ya uvuvi.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema hayo juzi, alipofanya ziara ya kikazi ya siku moja katika makao makuu ya taasisi hiyo iliyoko Jijini Dar es Salaam.

Alisema TAFIRI inategemewa katika kufanya tafiti za uvuvi kwa manufaaa ya sasa, yajayo na kuwafanya wavuvi kuwa na kipato endelevu ili shughuli hiyo ifanywe kitaalamu.

Ndaki alipongeza Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFISH), ambao umewezesha kujengwa jengo la maabara ya TAFIRI ambalo litaongeza wigo katika kufanya tafiti za uvuvi hapa nchini.

Alisema SWIOFISH imekuwa ikifanya kazi ya msingi na muhimu nje ya nchi na kuhakikisha fedha ambazo zimetolewa na Benki ya Dunia katika mradi huo zinasimamiwa vyema na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa TAFIRI, Dk. Ishmael Kimirei ,alimweleza Waziri Ndaki juu ya changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo, zikiwemo za vifaa vya maabara baada ya jengo la maabara kukamilika ambapo vifaa hivyo vinagharimu sh. bilioni 1.5.

Kutokana na ukosefu wa vifaa vya maabara, Waziri Ndaki alimuhakikishia mkurugenzi huyo kuwa, ataliwekea uzito jambo hilo kuanzia sasa na mwaka ujao wa fedha ili vipatikane vifaa hivyo na jengo hilo lifanye kazi ya utafiti pekee badala ya kuwa na vyumba vya ofisi.

Naye, mratibu wa mradi wa SWIOFISH, Nichrous Mlalila,alisema mradi huo wa miaka sita nchini unaotarajia kufikia tamati Septemba, mwaka 2022, umefadhiliwa na Benki ya Dunia na lengo ni kusimamia masuala ya uvuvi kuanzia ngazi ya utawala hadi kwa wavuvi pamoja ushirikiano kwa kikanda katika kuhakikisha unaboresha mnyororo wa thamani wa mazao ya uvuvi.

Scanned with CamScanner

**Jijini Dodoma, jana.** (Picha na Halima Kambi)



**WASHIRIKI wa Mkutano wa Wadau wa Sekta ya Mifugo, wakimsikiliza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alipofungua mkutano huo katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere, Dar es Salaam, jana.** (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu).

Scanned with CamScanner

# auzwa 30,000/

adaiwa kupelekwa kwa wafugaji... Endelea Uk. 2



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akitazama viatu alipotembelea banda la kiwanda cha Kilimanjaro International Leather Industries Company Limited kilichoko Karanga, Moshi, kabla ya kufungua mkutano wa wadau wa sekta ya mifugo kwenye Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere, Dar es Salaam, jana. Wa pili kulia ni Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki. **PICHA: PMO**

Scanned with CamScanner

# Ng'ombe wa serikali kuhesabiwa rasmi

Na Beatrice Shayo

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, ameagiza ng'ombe wote wa serikali kuingizwa kwenye mfumo wa utambuzi ili kusaidia kupata idadi ya mifugo nchini.

Waziri Ndaki aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa kiwanda cha kutengeneza hereni za kielekroniki za utambuzi wa mifugo nchini.

Alisema ng'ombe wa serikali katika maeneo mbalimbali wanatakiwa kuingizwa kwenye mfumo huo.

"Ni vizuri kuwa na mfumo mmoja utatusaidia kama nchi kwa kuwa tutatambulika kuwa tuna rasilimali za mifugo inayotoka Tanzania kiasi hiki... pamoja na ng'ombe wa serikali na wa watu binafsi tusiwe na utambulizi tofauti," alisema.

"Kuna baadhi ya watu wanatukodisha mashamba yetu wanasema wana ng'ombe kumbe hawana, tutajuaje hawana usajili, huu mfumo wa utambuzi utatusaidia kubaini mmiliki halali wa ng'ombe na wale wanaoiba mifugo."

Pia, Waziri Ndaki aliagiza ubadilishaji wa umiliki wa ng'ombe endapo mtu anataka kuuza mifugo yake ufanywe kwa haraka bila kuwapo na ucheleweshaji.

"Namna ya kubadilisha umiliki wa ng'ombe kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine unakuwa na mchakato mrefu kitu mbacho sisi wafugaji huwa hatupendi mara uende kwa mtendaji wa kijiji, mtendaji wa kata mara umtafute mtaalamu aweke taarifa kwenye kompyuta mara kompyuta ikosekane kijijini kunakuwa na mlolongo mrefu," alisema.

Alitoa wito kwa sekta binafsi kushiriki uwekezaji katika maeneo ya serikali hasa uzalishaji, mifugo na uvuvi ili kusaidia kuinua vipato vya wananchi.

"Sekta binafsi lazima muingilie kati ili kuongeza thamani ya mazao yetu ya mifugo watizame changamoto tulizonazo ili kutatua ni vizuri wakaiga mfano uliofanywa na hiki kiwanda," alisema.

Awali, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Hezron Nonga, alisema kuna maelekezo yalitolewa kwa ajili ya mifugo yote kutambuliwa na kusajiliwa.

Alisema mwaka 2017 walianza utambuzi kwa kupiga chapa jambo ambalo lililalamiwa kwa sababu chuma kilikuwa kinaunguza ngozi na kuonekana kwa alama.

Serikali kut

# RC Makalla kuvalia njuga maboresho mnada Pugu

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amesema atahakikisha anasimamia ipasavyo maboresho ya mnada wa Pugu na machinjio ili yaweze kuendana na hadhi ya jiji hilo baada ya kubaini kulega lega kwa suala hilo.

Aliyasema hayo jana jiji hapo baada ya kukutana na wadau wa sekta ya mifugo pamoja na Waziri Mashimba Ndaki, kujadili hali ya ubovu wa mnada huo, ambao mkandarasi anayeusimamia kuonekana kusuasua.

Alisema mazungumzo hayo yalikuwa na mafanikio makubwa baada ya Waziri Ndaki kumkabidhi jukumu la kumsimamia na kumbana mkandarasi amalize kazi ya kuboresha mnada huo baada ya kutoridhishwa na hali aliyoikuta wakati alipofanya ziara mnadani humo hivi karibuni.

Miongoni mwa changamoto zilizoonekana kuwapo katika mnada huo ni miundombinu mibovu inayohatarisha usalama wa mifugo pamoja na kasi isiyoridhisha ya mkandarasi aliyekabidhiwa kufanya marekebisho katika eneo hilo.

"Kwa sasa niahidi kuwa nitamsimamia ipasavyo mkandarasi ili kuhakikisha anakamilisha maboresho ya mnada kwa wakati na kupunguza changamoto zilizokuwa zikiwakabili wafugaji na wafanyabiashara katika eneo husika," alisema Makalla.

Pia, alisema endapo mnada huo utakuwa katika hali nzuri itasaidia pia machinjio ya kisasa ya Vingunguti kupokea mifugo yenye ubora utakaochochea upatikanaji wa nyama zenye ubora.

Miongoni mwa maboresho yanayotakiwa kufanyika katika mnada huo ni ujenzi wa uzio unaozunguka eneo husika, sakafu, eneo salama la kupakia ng'ombe, ujenzi wa vyoo na kero ya ukosefu wa maji. Mambo ambayo mkuu huyo aliahidi kusimamia mchakato wa utatuzi wake.

Scanned with CamScanner

LA HABARI TANZANIA

# HabariLEO

www.habarileo.co.tz

Habarileo | Habarileo | habarileo_tz | dailynews digital

VIJANA 600 WAITWA USAILI POLISI DODOMA UK.3

## WATENDAJI WAPEWA MAAGIZO 10 KUBORESHA MIFUGO UK.3

# Majaliwa: Mkachanje acheni maneno

HABARI KAMILI UK.2



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na wadau wa sekta ya mifugo kwenye mkutano uliofanyika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere, Dar es Salaam jana. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu).

## VIJANA WAWILI MBARONI WIZ WATOTO 11

- Waliwauza 25,000 hadi 30,000/- kwa wafugaji

JESHI la Polisi mkoa Mbeya linawashikilia watu watano kwa tuhuma mbalimbali wakiwemo wawili wanaotuhumiwa kujihusisha na

# Govt pushes for value-added livestock products

*Continued from page 1*

The Prime Minister implored relevant authorities to strengthen the production and distribution of quality livestock breeds, to increase productivity in the sector, while encouraging pastoralists to use quality breeds that have been researched and more productive.

He said the responsible ministry should strengthen extension services in the sector, so that pastoralists can get better knowledge on livestock keeping as well as strengthen livestock markets to enable pastoralists to sell their livestock at a better price.

Mr Majaliwa also called on the pastoralist communities to stop the practice of using children in cattle herding and instead, focus on ensuring that the children receive quality education for their future benefit.

He also warned pastoralists against driving their herds into farms, which tend to trigger conflicts.

"Pastoralists must understand that maize is for food and not a grazing field. You should learn to respect other people's economic activities," he said.

The premier instructed the Ministry of Livestock and Fisheries to fund research institutes in the country, for them to conduct productive research for the sector.

Earlier, the Chairperson of the Tanzania Pastoralists Association, Mr Jeremiah Wambura, appealed to the government to intervene in their standoff with game reserves, noting that there are over 5,000 cattle being held in game reserves, while pastoralists have won court cases.

"This is one thing that has hampered our activities. We request for your intervention in Burigi, Mkungunero and Meatu areas for authorities to release our cattle," he said The pastoralists requested the authorities to look for the best ways to conduct livestock operations, so that animal rights are observed.

The Minister for Livestock and Fisheries, Mashimba Ndaki said the aim of the meeting was to provide an opportunity for stakeholders in the private sector, to understand in detail the opportunities available in the livestock sector, gain joint experience and understand challenges and discuss how to overcome them.

Similarly, Mr Ndaki has called on LGAs to fund and involve pastoralists in the country to ensure 20 per cent of cattle are eligible for artificial insemination annually.

"Despite natural resources available in the county, the livestock sector is performing well below its potential. The livestock activities contribute 7.4 per cent to the country's GDP, through this conference will help strengthen activity in this sector and increase its contribution to GDP," he said.

Scanned with CamScanner

Broadband connectivity to reach all Tanzanians

DAILY NEWS Reporter



PRIME Minister Kassim Majaliwa admires leather shoes at the Kilimanjaro International Leather Industries Company (KLICL) booth during livestock sector stakeholders' meeting at Julius Nyerere International Conference Centre in Dar es Salaam yesterday. Second right is Livestock and Fisheries Minister Mashimba Ndaki. (Photo by PMO)

# Govt pushes for value-added livestock products

By HILDA MHAGAMA

THE government has issued ten directives to authorities, geared towards value addition in livestock and its products.

Top among the directives is for the councils to allocate 15 per cent of revenue collected from livestock activities and products, for the improvement of the sector.

Prime Minister Kassim Majaliwa issued the directives in Dar es Salaam yesterday, while opening a two-day meeting of livestock sector stakeholders in the country.

The premier also instructed stakeholders in the livestock sector to ensure that they depart from traditional livestock keeping and adopt modern methods in order to increase productivity, enhance herders' income and boost national economic growth.

"All Local Government Authorities (LGAs) should implement President Samia Suluhu Hassan's directives by allocating 15 per cent of revenue collected from the livestock sector in your areas, to be used in improving the sector which is crucial for poverty alleviation, food security and job creation," he noted.

Mr Majaliwa said establishing a public-private partnership in the sector was crucial to ensure that Tanzania's livestock sector plays an important role in fast-tracking the country's industrialisation drive.



**All Local Government Authorities should implement President Samia Suluhu Hassan's directives by allocating 15 per cent of revenue collected from the livestock sector...**

**– Majaliwa**

He said LGAs have the responsibility of working with livestock keepers in demarcation of surveyed land and give ownership of grazing areas according to traditional or legal procedures, in order to reduce persistent conflicts between herders and farmers, he said.

"Government officials and executives you must ensure that you work with the private sector, including pastoralists, in enabling them to invest and develop the setting up of livestock infrastructure including plunge dips, farm ponds and pastures," he noted.

Continues on Page [illegible]

Scanned with CamScanner

# Bukoba kusaka wezi wa ng'ombe

**Alodia Dominick**, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Bukoba**. Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Moses Machali ametangaza operesheni maalumu ya kuwasaka wezi wa ng'ombe.

Hatua hiyo inatokana na malalamiko ya wizi wa ng'ombe yaliyotolewa katika kikao cha Baraza la madiwani la halmashauri hiyo jana, ambapo madiwani walidai wezi hao hawachukuliwi hatua na vyombo vya dola.

Baada ya kusikiliza hoja za madiwani na alipopewa nafasi ya kuzungumza, Machali alitangaza operesheni hiyo itakayolihusisha Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na viongozi wa tarafa, vitongoji na wananchi.

Alisema ili kuwabaini wezi wa mifugo hiyo kutakuwa na mikutano ambayo wananchi watapiga kura ya siri kwa wanaodhani ni wezi.

"Nitoe tahadhari kwa madiwani, katika operesheni hiyo kuna ndugu zenu wanaweza kuhusishwa, hivyo sitaki diwani anifuate eti anataka kudhamini ndugu yake, malalamiko mmeyaleta ninyi, acha tushughulike na jambo ili tuwanase, kwa kuwa wanaikosesha jamii amani, wananchi watapiga kura ya siri kuwabaini wezi wa ng'ombe, kwa yule atakayepata kura nyingi tutaanza kumfuatilia," alisema Machali.

Diwani wa kata ya Bujugo ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Prinatus Anatory alisema aliibiwa zizi lote la ng'ombe ambalo lilikuwa na mifugo tisa, alitoa taarifa kituo cha polisi lakini mifugo haikupatikana hadi leo na hakuona hatua zilizochukuliwa kuwasaka wezi hao.

Alisema iwapo itafanyika operesheni hiyo itasaidia kubaini mtandao mzima wa wezi hao kwa kuwa unaonekana ni mkubwa na inasemekana mtandao huo unasafirisha ng'ombe hao nje ya nchi na wengine wanawachinja na kuwauza hapa nchini.

Hata hivyo, takwimu za ng'ombe walioibwa hazikupatikana mara moja kutokana na taarifa za wizi kutolewa kwenye uongozi wa kata na nyingine kituo cha polisi.

Wakati huohuo, mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Fatina Laay alisema halmashauri hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 inatarajia kukusanya Sh35.4 bilioni ambapo kwa mwaka 2020/2021 ilitarajia kukusanya Sh35.9 bilioni, lakini walikusanya Sh30.5 bilioni.

"Nawaomba ndugu zangu madiwani tushirikiane katika kuhamasisha wananchi kulipa kodi, kubuni vyanzo vipya vya mapato na kudhibiti matumizi yetu ili tupige hatua zaidi katika maendeleo ya halmashauri yetu na taifa," alisema.

Scanned with CamScanner




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akikagua mkanda uliotengenezwa kwa ngozi wakati wakipewa maelezo na Ofisa wa Masoko wa Kiwanda cha Kilimanjaro International Leather, Fredrick Njoka (kulia) alipotembelea banda lao kabla ya kufungua mkutano wa wadau wa sekta ya mifugo ulilofanyika kwenye Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere jijini Dar es Salaam jana. **Picha na Sunday George**

# 'Wafugaji msiwape watoto kuchunga'

**Bakari Kiango**, Mwananchi
bkiango@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa amekemea vitendo vya baadhi ya wafugaji wanaowapa watoto ng'ombe kuwachunga, akisema si sahihi kwa sababu hawana uwezo wa kukaa na kundi kubwa la mifugo.

"Tuache tabia ya kuwapa watoto wadogo kuchunga ng'ombe, kwa sababu wanatakiwa kwenda shule, pili hawana uwezo wa kukaa na kundi kubwa. Najua utamaduni huko hivyo, lakini tuweke mwelekeo mzuri wa ufugaji," alisema Majaliwa.

Majaliwa alitoa kauli hiyo jana, wakati akifungua mkutano wa wadau wa sekta ya mifugo ulioandaliwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mkutano uliwashirikisha baadhi wa wakuu wa mikoa ya Tanga, Pwani, Iringa, Lindi, Dar es Salaam, Manyara na Tabora.

Aliwataka wafugaji kuwakabidhi mifugo vijana wenye uwezo wa kutafakari na kujua namna ya kutekeleza vyema shughuli ya kuchunga na endapo ng'ombe akienda ndivyo sivyo, ni rahisi kumrudisha katika njia yake.

Katika mkutano huo, Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT), Jeremiah Wambura alimuomba Majaliwa kuingilia kati sakata la ng'ombe 5,000 wanaoshikiliwa katika hifadhi mbalimbali, zikiwamo za Meatu na Burigi, licha ya Mahakama kuamuru ziachiliwe.

"Tunaomba utusaidie mifugo hii iachiwe kwa sababu ng'ombe wanashikiliwa huku ndama wanaachwa wakifa. Waziri Mkuu, hatuwezi kupata maziwa kama ng'ombe wanashikiliwa," alisema Wambura.

Akijibu ombi hilo, Majaliwa alisema, "kama Mahakama imesema ng'ombe hawana hatia waachiwe ili mfugaji achukue mfugo wake na kujipanga vizuri katika maeneo yake.

Kama kuna mfugaji hapa ng'ombe wake wameshikiliwa baada ya tamko hili wamuone waziri," alisema Majaliwa.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alimuomba Majaliwa kuagiza wakuu wa mikoa kutekeleza waraka wa mwaka 2002 unaoelekeza halmashauri kutenga asilimia 15 ya mapato yanatokanayo na mifugo, kisha zitumike kuboresha sekta hiyo.

"Huko Lindi juzi wakulima wawili wameuawa na wafugaji, sio jambo jema, sababu ng'ombe amepelekwa katika shamba la mahindi. Ni vizuri kila mmoja aheshimu shughuli ya mwenzake ili tuishi vizuri katika jamii yetu."
Kassim Majaliwa

Scanned with CamScanner

# Wahimizwa kuchangamkia kuuza nyama Saudi Arabia

**Na Oscar Job**

SERIKALI kupitia kwa Masajili wa Bodi ya Nyama (TMB) imesema imejipanga kutumia soko la nyama la nchi ya Saudi Arabia na hivyo kuwataka wafugaji na wafanyabiashara kuitumia fursa hiyo kuboresha mifugo yao ili kujiinua kiuchumi.

Akizungumza na HabariLEO jana, Msajili wa TMB, Dk Daniel Mushi alisema kwa kipindi kirefu Tanzania imekuwa ikitumia fursa za masoko ya nyama yanayopatikana katika mataifa mbalimbali duniani na kwamba ujio wa soko la Saudi Arabia ni fursa adimu ya kuchangamkia.

Mwishoni wa wiki, Balozi wa Tanzania nchini Saudi Arabia, Ali Jabir Mwandimi alibainisha kuwa hivi karibuni Tanzania itarejea tena katika usafirishaji wa nyama kwenda nchini humo ikiwa ni takribani miaka 19 tangu kusitishwa kwa kibali kilichokuwa kinaruhusu nyama kutoka Tanzania kuingia nchini humo.

"Bodi tumejipanga kikamilifu kuhakikisha tunaitumia ipasavyo fursa hiyo na zingine za biashara za nyama. Kikubwa nitoe rai kwa wafugaji wote nchini kuitumie nafasi hii kwa kuzingatia matakwa ya soko," alisema.

Alisema soko la nyama la nje ya nchi linahitaji mifugo yenye ubora na iliyokidhi vigezo mbalimbali vinavyoendana na mahitaji ya soko husika huku akisisitiza kuwa jambo la muhimu ambalo kama serikali imelichukua ni kuhakikisha wafugaji wanainenepesha mifugo hiyo ili iweze kufikia viwango vinavyohitajika katika soko la kimataifa.

Dk Mushi alisema katika kulizingatia hilo, bodi hiyo kwa kushirikiana na halmashauri mbalimbali nchini zimeendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya unenepeshaji wa mifugo yao ili kuiwezesha kuwa na ubora ule unaohitajika ili iweze kupata soko katika mataifa hayo.

Alisema kwa sasa Tanzania inauza nyama katika mataifa ya Oman, Qatar, Dubai, Comoro na baadhi ya nchi zilizopo katika bara la Afrika.

Alisema katika kipindi cha mwaka jana Tanzania ilifanikiwa kuuza wastani wa tani 1,774 za nyama nje ya nchi.

Scanned with CamScanner

# Majaliwa atoa maagizo 10 kuboresha mifugo

Na Halima Mlacha

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ametoa maagizo zaidi ya 10 kwa mamlaka za serikali likiwamo la kutekeleza Waraka wa Rais namba moja kwa kutenga asilimia 15 ya mapato yatakanayo na sekta ya mifugo katika halmashauri zitumike kuboresha zaidi sekta hiyo.

Waziri Mkuu pia amekemea tatizo la migogoro baina ya wafugaji na watumiaji ardhi wengine linalosababisha mauaji yanayozuilika.

Alitoa maagizo hayo Dar es Salaam jana wakati akifungua mkutano wa siku mbili wa wadau wa sekta ya mifugo nchini.

"Ninatoa maelekezo kwa mamlaka za serikali za mitaa, na leo (jana) wakuu wa mikoa mko hapa, hakikisheni mnatekeleza Waraka wa Rais namba moja wa mwaka 2022 kwa kutenga asilimia 15 ya mapato yatokanayo na mifugo na kuweka katika uboreshaji wa sekta ya mifugo," alisema. Majaliwa alizitaka mamlaka za serikali za mitaa kuzisimamia halmashauri zitenge asilimia hizo 15.

Aliwaagiza viongozi na watendaji wa serikali kua karibu na sekta binafsi na wafugaji ili kuwawezesha waendelee kuwekeza kwenye sekta hiyo.

Pia aliziagiza mamlaka za serikali za mitaa kushirikiana na sekta binafsi wakiwemo wafugaji katika kutenga, kupima, kusimamia na kuendeleza maeneo ya malisho.

Alisema mamlaka hizo zina wajibu wa kusimamia wafugaji kuongeza tija katika uzalishaji kupitia uhamilishaji, upandishaji wa madume na mitamba bora.

Aidha, aliitaka Wizara ya Mifugo na Uvuvi kutumia taasisi za utafiti na kuzipatia fedha zifanye tafiti zenye tija kwa sekta ya mifugo na kuimarisha taasisi zinazozalisha mbegu bora za kisasa pamoja na kuhamasisha wafugaji watumie mifugo bora iliyofanyiwa utafiti na kuonesha kuwa na tija zaidi.

"Pia naagiza wizara isimamie na kuimarisha mfumo wa masoko ya mifugo na wafugaji wauze mifugo yao kwa bei nzuri ikiwamo kuimarisha ushirika wa wafugaji ili wafugaji waweze kufikiwa waunde umoja wao wachanganue changamoto zao badala ya kila mmoja kuwa sehemu yake hivyo kuwa ngumu kuwafikia," alisema Majaliwa.

Aliiagiza Wizara ya Mifugo kushiriki kikamilifu katika kutatua migogoro inayowahusu wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

"Hakikisheni wafugaji wanaelimishwa na kuhamasishwa kufuga kulingana na maeneo waliyonayo. Halmashauri nazo zihamasishe ufugaji ambao hautochochea migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi," alisema Majaliwa.

Aliagiza ng'ombe zaidi ya 5,000 wanaoshikiliwa katika hifadhi mbalimbali nchini, wizara kufuatilia na endapo mahakama imeamuru waachiwe, waachiwe mara moja.

Alitaka pia operesheni za mifugo nchini kufanywa kwa weledi, lakini pia akiwasisitizia wafugaji waepuke shughuli za ufugaji kwenye maeneo yasiyoruhusiwa hususani vyanzo vya maji, hifadhi na maeneo mengine ikiwemo ya kilimo.

Aliagiza mikoa yote kufanya sensa ya mara kwa mara ya mifugo ili kufahamu ipo mingapi na iko wapi.

Alisema sekta ya mifugo ni muhimu na ya kipaumbele kwa Serikali ya Awamu ya Sita ikiwa na lengo la kuiwezesha kuchangia ipasavyo katika kuwakwamua wananchi kiuchumi na kutoa malighafi ya kwa viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo.

Majaliwa pia alitoa wito kwa wafugaji kuacha tabia ya kuwapa watoto kazi ya kuchunga mifugo badala yake wajikite katika kuhakikisha watoto hao wanapata elimu bora kwa manufaa yao ya baadaye.

Aidha, aliwataka kujikita katika ufugaji wenye tija utakaohakikisha malighafi zinazotokana na mifugo kama vile nyama, maziwa na ngozi zinapatikana kwa wingi lakini pia kwa ubora unaoweza kupata soko kubwa ndani na nje ya nchi.

Alisema kwa sasa uzalishaji wa bidhaa za mifugo bado uko chini kuanzia nyama, maziwa na hususani ngozi ambazo zimeharibiwa na kuwekwa chapa na kuandikwa majina.

"Serikali iko nyuma yenu, hakikisheni mnafuga kwa kuzingatia utaalamu unaotolewa. Rais alitoa maagizo ya kuongeza uzalishaji wa nyama kutoka kilo 730,000 mwaka huu na kufikia 940,000 mwaka 2025/26.

Alisema malengo mengine ni maziwa kuongezeka kutoka lita bilioni 3.1 mwaka huu hadi lita bilioni 4.5 mwaka 2025/26 na ngozi kutoka tani 16 mwaka huu hadi tani 25 mwaka 2025/26.

Alihimiza kuhusu umuhimu wa wafugaji kutumia fursa ya masoko kwa kuwa mataifa mengi yanahitaji nyama kutoka Tanzaia.

Scanned with CamScanner